

BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI



DIRISHA LA MAREKEBISHO - MKUPUO WA MACHI, 2026

Baraza linapenda kuvijulisha vyuo vyote vilivyoruhusiwa kutoa mafunzo kwa mkupuo wa Machi 2026 kuwa Baraza limefungua dirisha la kufanya marekebisho na kuwasilisha upya taarifa za waombaji zilizokuwa na makosa au upungufu katika dirisha la awali la udahili.

Dirisha la marekebisho litakuwa wazi kuanzia tarehe **22 hadi 26 Aprili, 2026**.

Vyuo vyote vinahimizwa kukamilisha zoezi hili ndani ya muda uliopangwa ili kuwezesha hatua zinazofuata za mchakato wa udahili.

Uhakiki wa taarifa zilizorekebishwa utafanyika kuanzia tarehe **27 Aprili hadi 4 Mei, 2026**, na majibu ya uhakiki yatatolewa rasmi tarehe **10 Mei, 2026**.

Baraza linasisitiza vyuo kuzingatia muda uliotolewa ili kuhakikisha mchakato wa udahili unakamilika kwa ufanisi, uwazi na kwa wakati.

Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Masoko – NACTVET

22 Aprili, 2026